**FILEMONI**
**MTAALA**

I. **MAELEZO KWA UJUMLA**.

A. Mwalimu: Roy C. Deaver
B. Mkalimani: Chris Mwakabanje
C. Kila darasa linachukua takribani dakika 38.

II. **MAELEZO NA MALENGO**.

A. Kujifunza kwa kina Waraka kwa Filemoni.
B. Mkazo utatiliwa katika maeneo ambayo kuna kanuni za kuzitendea kazi.
C. Mwanafunzi atajifunza upendo wa Mungu kwa mwanadamu (watumwa na walio huru), kuona Mungu kupitia majaliwa yake akiwa kazini katika maisha ya Wakristo hawa, na kuelewa majukumu maalum ambayo kila Mkristo anayo.

III. **VIFAA VINAVYOHITAJIKA WAKATI WA KUJIFUNZA**.

A. Unapaswa uwe na vitu vifuatavyo:
1. Biblia (swahili – UV, English – ASV, KJV, NKJV).
2. Masomo kwa video.
3. Maelezo (Notes) ya kozi hii.

B. Maoni: Tunapendekeza uwe na fafanuzi (commentary) yoyote yenye kushikilia mafundisho ya awali (conservative) katika Filemoni.

IV. **MAMBO YA KUFANYA KATIKA KOZI HII**:

A. Usome kitabu chote cha Filemoni angalau mara tano.
B. Angalia kikamilifu katika video masomo yote.
C. Usome kikamilifu notisi zote za darasani.
D. Kamilisha kazi yote ya kudondoa (maelezo yapo chini).
E. Wasilisha makala ya muhula (maelezo hapo chini).
F. Hakikisha unafanya mtihani mmoja.
G. Ni sharti uwe na jumla ya wastani wa maksi angalau 70.

V. **KAZI YA KUDONDOA**.

A. Mistari ya kudodoa lazima iandikwe (au ichapwe) bila kutazamia mahali, kisha itumwe VBI kwa masahihisho. Mistari ni lazima itoke katika UV kama ulivyoonyeshwa katika fomu yako ya maombi ya kujiunga na VBI.

B. Mistari yote ni sharti iandikwe ama kuchapwa kwa mkao mmoja (mara moja). Unaweza kujifunza zaidi na kuianza upya yote iwapo ulikosea, lakini unatakiwa kuanza upya yote na kuiandikwa katika mkao mmoja.

C. Kwa kozi hii, mistari ifuatayo unapaswa kudondoa:
Filemoni 4-7 Filemoni 10-11 Filemoni 15,16
Filemoni 21,22

D. Kazi ya kudondoa uiwasilishe VBI wakati unatuma mtihani wako wa tatu.

E. Maoni: Njia bora ya kudondoa ni kuandika mistari katika vijikadi ili kwamba iwe rahisi kwako kuipitia mara kwa mara muda wote unavyoendelea na kozi hii.

**VI. MITIHANI.**

A. Kuna mtihani mmoja wa kufanya katika Filemoni.

B. Unapokaribia mwisho wa kitabu, wasiliana nasi na kuomba mtihani.

C. Ukishapokea mtihani, unaruhusiwa kuupitia na kujifunza.

D. Lakini, unapofanya mtihani, unatakiwa uufanye kikamilifu bila kutazama kwenye notisi, Biblia, kitabu, n.k.

**VII. MAKALA YA MUHULA.**

A. Andika makala juu ya muhtasari wa Filemoni ukielezea mambo muhimu katika kila sura na kutoa masomo ambayo tunaweza kujifunza.

B. Makala unapaswa uiandikie fafanuzi (commentary) ya mstari kwa mstari wa kitabu cha Filemoni mistari yote 25. Maoni yazingatie moja au zaidi ya mambo yafuatayo: maelezo ya mstari, maana ya neno la ufunguo la Kiyunani katika mstari, msaada rejea katika Biblia sehemu nyingine, somo tunalojifunza kutoka katika mstari, au jinsi gani mstari unaweza kutumika kwetu.

C. Makala itatakiwa unapotuma mtihani wako wa mwisho VBI pamoja na dondoa.

**VIII. MAKSI.**

A. Kazi ya kudondoa, makala ya muhula, na mitihani itasahihishwa tofauti tofauti.
B. Maksi za mwisho zitazingatia juu ya wastani wa kazi zako zote ulizopewa.
C. Unaweza kuomba ili ufafanuliwe na kufikiriwa juu ya maksi, lakini kwa vyovyote vile VBI ndiyo itakuwa na uamuzi wa mwisho.

IX. **TUNZO**.

A. Tunzo itatolewa, ikiwa ni pamoja na cheti, pale tu utakapokuwa umefanikiwa kumaliza kazi yako kikamilifu, kanda za video umerejesha (kama uliziazima), na ada yote kwa kozi hii umelipa.

B. Mungu na abariki jitihada yako ya kujifunza neno lake lenye uvuvio!

**UTANGULIZI**

Kitabu cha Filemoni ni waraka mfupi wenye sura moja lakini wenye ujumbe muhimu sana katika Agano Jipya, tuliopewa na Roho Mtakatifu, kilichoandikwa na mtume Paulo, kuwa hazina kwao wanaochukua muda wao kutafakari juu ya ujumbe huu muhimu.

Katika waraka huu mdogo mzuri tunaona: (1) Mungu (kupitia Roho Mtakatifu) kama mwandishi; (2) mtume Paulo (kama mwandishi aliyevuviwa); (3) Filemoni (kama mtu aliyeandikiwa, mmiliki wa mtumwa aliyekimbia); (4) Onesimo (aliyemkimbia Filemoni, ambaye alikwenda Rumi, ambako alikutana na Paulo, na kuletwa kwa Kristo na Paulo, katika Rumi). Kulingana na mapenzi ya Mungu, Paulo alikuwa akimrejesha Onesimo kwa Filemoni.

**MCHANGANUO WA MAONI KATIKA KITABU CHA FILEMONI**

I. Mwandishi? Roho Mtakatifu.

II. Mwandishi? Paulo, mtume wa Yesu Kristo.

III. Uliandikwa kutoka wapi? Rumi, ambako Paulo alikuwa amefungwa.

IV. Aliandikiwa nani? Filemoni, aliyekuwa na mtumwa.

V. Uliandikwa lini? 62 B.K. Moja ya nyaraka nne za gerezani (Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, na Filemoni).

VI. Kwa nini waraka uliandikwa?

Onesimo alikuwa mtumwa, aliyemilikiwa na Filemoni wa Kolosai. Onesimo alitoroka, hata kufika mji wa Rumi, na huko akakutana na mtume. Kupitia Paulo, Onesimo alifanyika kuwa Mkristo. Paulo akawa katika hali ya kujali sana mtu huyu, na akataka Filemoni awe naye – lakini asingefanya hivyo bila ya idhini ya Filemoni. Kwa hiyo, Paulo alimrejeza Onesimo kwa Filemoni, akiungana na Tikiko (Angalia Kol.4:7-9), na kuandika barua maalum kwa niaba yake. Paulo alimsihi kumpokea Onesimo "kama ndugu," na kubainisha imani aliyokuwa nayo kwa Filemoni <u>angefanya hivyo na kuzidi</u>! Paulo aliandika akimwomba Mkristo amkubali Onesimo.

## MAELEZO WA UFUNGUO WA KITABU CHA FILEMONI

KUSUDI:

Kumwomba Mkristo amkubali Onesimo; kufanya upatanisho wa kweli baina ya Filemoni na Onesimo na wakati huo huo, kuupatia ulimwengu baadhi ya mambo muhimu na masomo mazuri ajabu kutoka kwa Mungu kwa wanadamu.

I. Paulo anabainisha shukrani zake kwa Filemoni (mstari wa 1-10), na

II. Anamsihi Filemoni amkubali Onesimo kama Mkristo (mstari wa 11-25).

## MAELEZO KWA UFUPI

I. Paulo anatoa salaam (1-3);

II. Anaeleza shukrani zake kwa Filemoni (4-7);

III. Anabainisha kusudi lake la kuandika (8,9);

IV. Anabanisha hisia zake juu ya Onesimo (10-16);

V. Anafunua haja yake (17-20);

VI. Anaeleza imani yake kwa Filemoni kwamba angefanya zaidi ya alivyoombwa (21);

VII. Anaeleza imani yake kuwa yeye (Paulo) angemtembelea Filemoni muda si mrefu (22).

VIII. Anatuma salaam kutoka kwa watu ambao alikuwa nao (23,24);

IX. Anahitimisha kwa sala (25).

Zingatia: Tunapendekeza kujifunza sehemu hizo tisa kwa makini zaidi.

## FAFANUZI – FILEMONI

I. Salaam, mstari wa 1-3.

A. Paulo anarejea katika kiini cha barua.

1. Paulo, mfungwa wa Kristo Yesu, na
2. Timotheo ndugu yetu.
3. Linga. Flp.1:1; Kol.1:1.

B. Paulo anatoa maelezo maalum kwao anaowaandikia:
1. Kwa Filemoni:
   a. “Ndugu mpendwa;”
   b. “Mtenda kazi pamoja nasi.”

2. Kwa Afia:
   a. “Ndugu yetu” (sister).
   b. Pengine mke wa Filemoni.

3. Kwa Arkipo:
   a. “Askari mwenzetu.”
   b. Pengine mtoto wa Filemoni na Afia.
   c. Angalia: Kol.4:17.

4. “Kwa kanisa lililo katika nyumba yako.”
   a. Angalia kwamba kanisa lilikutana ndani ya nyumba ya Filemoni;
   b. Angalia pia: Onesimo alimilikiwa na Filemoni; Onesimo alikuwa mwenyeji wa Kolosai, Kol.4:9. Ni dhahiri, basi, lilikuwa ni kanisa la Kolosai lililokusanyika nyumbani kwa Filemoni.

C. Paulo anabainisha ombi lenye sala.
1. Paulo anaomba neema ya Mungu na amani yake ijayo baada ya neema kuwa juu yao.
2. Neema na amani hutoka kwa Mungu Baba, na kwa Bwana Yesu Kristo.

D. Uchanganuzi:
1. Filemoni na familia yake ni dhahiri walikuwa watu walioonekana kuwa na uwezo wa mambo ya mwili, na walikuwa wakitumia uwezo wao wa mali kwa utukufu wa Mungu.
2. Hawa walifanyika kuwa Wakristo na wakawa na shauku ya kuineza injili kwa watu wengine.
3. Filemoni, pamoja na Lidia, walikuwa wakarimu, walitoa nyumba zao kwa ajili ya kanisa kukusanyika humo.
4. Lazima daima tuitafakari neema ya Mungu, na amani yake ijayo baada ya neema.

II. “Namshukuru Mungu…” (mistari ya 4,5).

A. Paulo anataja shukrani zake kwa Filemoni.

B. Anabainisha kwamba “siku zote” ametoa shukrani zake.

C. Anaeleza kwamba <u>ametoa</u> shukrani zake <u>mbele za Mungu</u>.

D. Ameelezea kwamba daima ametoa shukrani <u>kupitia sala zake.</u>

E. Paulo anataja kwamba alikuw siku zote akimshukuru Filemoni kwa sababu ya <u>upendo</u> na <u>imani</u> yake, ambayo ailikuwa akiidhihirisha.
1. Mbele za Bwana, na
2. Mbele za watakatifu wote.

F. Uchanganuzi:
1. Paulo wakati wote aliwashukuru Wakristo Waaminifu.

   2. Paulo "siku zote" alimkumbuka mtu mmoja mmoja katika sala na makusanyiko katika sala zake.
   3. Wakristo ni lazima tuwe na tabia ya upendano wa ndugu.

III. "…Ili…" mstari wa 6.

A. Paulo anataja kusudi la haja yake kwa Filemoni.

B. Aliomba ili kwamba "ushirika" wa imani ya Filemoni (kama ilivyodhihirika) ingehamasisha maarifa ya mema yote tunayopaswa kuwa nayo katika Kristo.

C. Uchanganuzi:
   1. Imani ya Mkristo lazima idhhiirike kwa njia maneno na matendo.
   2. Filemoni alikuwa akiyatendea kazi mambo aliyofundisha Bwana. Alikuwa akionyesha ushawishi wa Mkristo sahihi (Math.5:16).

IV. "…Furaha na faraja…" mstari wa7.

A. Paulo anataja kuwa alikuwa na furaha na faraja kubwa katika upendo wa Filemoni.

B. Hii ni kwa sababu upendo wa Filemoni ulidhihirika kwa namna ya kuwashangaza wengine.

C. Na hiyo ndiyo sababu upendo wa Filemoni uliburudisha mioyo ya watakatifu.

D. Uchanganuzi:
   1. Maisha ya Mkristo ni yenye kushirikiana na wengine.
   2. Ni lazima impendeze Mungu mwenyewe mtu anapokuwa Mkristo:
      a. Kudhihirisha kujali wazi mahitaji ya watu wengine:
      b. Kuburudisha mioyo ya watakatifu.

V. "…Nakusihi lakini…" mistari ya 8-10.

A. Paulo anataja kwamba mamlaka yake "katika Kristo" angeweza kumwamuru Filemoni kufanya mambo yaliyo sahihi.

B. Alisita, hata hivyo, kwa sababu ya mwenendo wa upendo alioona:
   1. Kwamba asiamini mtu, bali,
   2. Amsihi Filemoni.

C. Hivyo basi, anamsihi Filemoni kama:
   1. Paulo mzee kiumri; na
   2. Paulo, mfungwa wa Kristo Yesu.

D. Anamsihi filemoni kwa niaba ya mtu fulani:
   1. "Mwanangu,"
   2. "Niliyemzaa katika vifungo vyangu,"
   3. Yaani, "Onesimo."

E. Uchanganuzi:
   1. Paulo alikuwa na mamlaka ya kuamuru. Alikuwa ni mtume wa Yesu Kristo, wakili wa mfalme. Mambo aliyoamuru na kufundisha lazima yazingatiwe!
   2. Paulo alikuwa mwangalifu katika kuyatumia madaraka yake. Ni rahisi kuyatumia vibaya mamlaka. Mamlaka kwa asili huhusisha wajibu wa matumizi wa kuyatumia mamlaka kulingana na mapenzi ya Mungu.
   3. Paulo alikuwa na upendo, mnyenyekevu na mwema. Mara nyingi alitumia neno "kusihi" – neno lenye kuonyesha upendo, utu wema na unyenyekevu.

4. Upendo mkuu wa Paulo, kujali, unyenyekevu (Ukristo) umedhihirika kwa kujisumbua kwake kwa ajili ya wengine – kumsaidia mtu mwingine (linga. Gal.6:10).
5. Kama vile Onesimo alivyokuwa na Paulo akimwombea, tunaye Kristo yeye mwenyewe akituombea mbele ya kiti cha enzi cha neema. "Naye kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai siku zote ili awaombee (Ebr.7:25). "Na kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki" (1 Yoh.2:1).

VI. Onesimo, mistari ya 10-14

A. Paulo alimsihi Filemoni kwa niaba ya Onesimo.

B. Amemwita Onesimo "mtoto wake.:

C. Anataja kuwa walimwongoa Onesimo alipokuwa (Paulo) gerezani.

D. Amemwelezea Onesimo kuwa zamani alikuwa "hamfai" Filemoni, lakani kwamba sasa "alimfaa" katika maeneo mawili"
1. Kwa Filemoni, na
2. Kwa Paulo.

Zingatia: Hivi ndivyo maana ya neno "Onesimo" yaani "msaada, anayefaa."

E. Paulo anaelezea:
1. Kwamba alimrejeza Onesimo kwa Filemoni, na
2. Kwamba kwa kufanya hivyo alikuwa akiutuma moyo wake mwenyewe.

F. Alisisitiza kwamba (Paulo) alitaka kubaki na Onesimo:
1. Huyo Onesimo angeweza kumtumikia (Paulo) badala ya Filemoni, lakini
2. Kwamba asingefanya hivyo bila ya idhini ya Filemoni ili kwamba wema wa Filemoni uwe kwa "hiari," na isiwe kwa lazima.

G. Uchanganuzi:
1. Onesimo ni mmoja ya ushahidi wa uchapaji wa kazi wa Paulo usiokoma. Ingawa alikuwa mfungwa, Paulo aliendelea kufundisha, na juhudi yake ilipata thawabu. Hatupaswi kukoma kufundisha na kuhubiri injili. Na kazi yetu haitakuwa bure (1 Kor.15:58).

2. Ingawa Onesimo alikuwa mtoto wa kiroho wa Paulo, Onesimo hakumwita Paulo "Baba Paulo." Ndugu wa Korintho hawakumwita "Mkulima Paulo" (linga. 1 Kor.3:9) au "Mjenzi Paulo" (1 Kor.3:10ff). Ndugu wa Thesalonike hawakumwita "Mlezi Paulo" (1 Thes.2:7).

3. Uongofu unafanya mtu kutoka upande wa "asiyefaa" kuingia ukurasa wa "anayefaa."

4. Suala la Onesimo linaonyesha kwamba uongofu unamfanya mtu afanye matengenezo (marekebisho, kuweka mambo sawa) kwa kadiri iwezekenavyo.

5. Ikiwa Onesimo angeweza kumhudumia Paulo badala ya Filemoni (mstari wa 13), basi kuna angalau baadhi ya mambo ambayo mtu anapofanya kupitia mtu mwingine, hufanya mwenyewe (linga. 2 Kor.8:23; Lk.10:33-37).

6. Paulo alijali suala la kufanya mambo kwa njia ya heshima (linga. 2 Kor.8:20,21; Rum.12:17). Hakutaka msaada wa "mahitaji" kutoka kwa Filemoni, bali tu msaada wa "hiari." Mungu ana mtazamo huo huo juu ya utoaji wetu (2 Kor.9:7).

7. "Wema" si tu ni tabia, bali tendo au matendo. Utumishi wa Filemoni kwa Paulo kwa njia ya Onesimo ungekuwa ni "wema" wa Filemoni (mstari wa 14).

VII. "…Kwa muda…" mstari wa 15,16.

A. Paulo anaelezea kwamba "pengine" Onesimo alitengwa na Filemoni "kwa muda" ili kwamba Filemoni aweze kuwa naye "milele" – si kama mtumwa, bali kama ndugu mpendwa katika Kristo.

B. Katika kurejea kwake, Onesimo angekuwa "mtumishi" na zaidi ya kuwa mtumishi.

C. Angakuwa "ndugu."
1. Haswa akiwa mpendwa wa Paulo, na
2. Hata kuwa kipenzi kwa Filemoni – katika mambo mawili:
   a. Kama mtumishi , na
   b. Kama Mkristo mwenzi.

D. Mchanganuo:
1. Hapa tunaona rejea ya ajabu juu ya majaliwa ya Mungu, maana ikiwa Paulo hapa anasema haikuwezekana kabisa, basi pasingekuwa na maana ya kuelezea maneno haya. Basi, fungu la maneno linaonyesha:
   a. Ukweli wa majaliwa ya Mungu;
   b. Imani ya Paulo katika majaliwa ya Mungu; na
   c. Jinsi gani Mungu anaweza na kufanya kazi kupitia wanadamu na mambo yao.

2. Angalia usawa utokanao na ushawishi wa injili ya Kristo. Ujumbe huo huo unakwenda kwa watu wote. Wote wanasimama wakiwa sawa mbele za Mungu. Wakristo wote ni "familia" moja. Wote ni ndugu na dada katika Kristo."

VIII. "…Mpokee…" mstari wa 17

A. Hapa ni moja ya ufunguo wa kitabu. Paulo anamsihi Mkristo ampokee Onesimo.

B. Paulo anamwambia Filemoni: "Kama ukiona mimi kuwa mshirika nawe, mpokee huyu (Onesimo) kama mimi mwenyewe."

C. Uchanganuzi:

Jinsi Filemoni angempokea Onesimo ingedhihirisha wazi uhusiano wake na Paulo. Namna hiyo, mwitiko wetu juu ya maagizo ya Bwana ni dhahiri jinsi tabia zetu zilivyo mbele zake, kadhalika mbele za Baba. Linga. 1 Yoh.5:3; Yoh.5:3; Yoh.14:15.

IX. "…Ukiandike hicho juu yangu…" mstari wa18.

A. Paulo anatoa nafasi iwapo Onesimo alikuwa amemfanyia jambo "baya" Filemoni, au "kumwia" kitu.

B. Neno "kama" (katika Kiyunani Agano Jipya) linaonyesha ukweli juu ya hali hiyo. Ukubwa wa kosa ungetegemea pengine kwa sehemu kubwa juu ya nia ya Filemoni na madai – hasara na gharama ambazo "aliyekimbia" na wasaa wa kutokuwepo.

C. Paulo anasema: "Na kama hivyo ndivyo, basi nidai mimi."

D. Paulo anasisitiza:
1. Ukiandike hicho juu yangu.
2. Mimi Paulo nimeandika kwa mkono wangu mwenyewe.
3. Mimi nitalipa.

E. Uchanganuzi:
   1. Kama vile Paulo alivyosihi juu ya suala la Onesimo, na hata kuwa tayari kuchukua deni la Onesimo, sawa na Kristo alivyofa juu yetu, akalipa deni letu. “Yesu alikufa na kulipia; msalabani Kalvari.”

   2. Paulo alitaka ushirika kamili na timilifu baina ya Filemoni na Onesimo. Hili lingetokea kama pangefanyika toba ya kweli kwa upande wa Onesimo, na msamaha wa kweli upande wa Filemoni. Ni lazima tupende na kuwa tayari kurekebisha makosa yetu. Lazima tuwe na msamaha.

X. “…Nakuwia hata nafsi yako…” mstari wa 19.

A. Paulo anamkumbuka kwa upole (ingawa anabainisha wazi) kwamba Filemoni mwenyewe anawiwa na Paulo.

B. Jambo hili anarejea ukweli kwamba Paulo alimwongoa Filemoni, pengine alipokuwa Efeso.

C. Uchanganuzi:
Sisi – kwa njia maalum – tunawiwa na watu waliotufundisha ukweli na kutoongoza kwa Kristo.

XI. “…Uniburudishe…” mstari wa 20.

A. Tena Paulo anamsihi Filemoni kuwa atafanya mambo aliyomwomba afanye.

B. Ili kuwaona Filemoni na Onesimo wamepatana kabisa, kama ndugu katika Bwana, kungekuwa na fursa ya kuburudika kwa Paulo. Kufikia hapa, Filemoni angempokea na kumsamehe. Paulo anaomba: “Uniburudishe moyo wangu katika Kristo.”

C. Uchanganuzi: Wakristo lazima watamani na kufurahia “kumpokea mtu na kumsamehe.”

XII. “…Utafanya zaidi ya hayo…”

A. Paulo anaonyesha imani kwa Filemoni kwamba angefanya hivyo.
   1. Si tu mambo aliyoombwa, bali
   2. Hata zaidi ya yalioombwa.

B. Pengine hili Paulo ana maana kwamba Filemoni angemwachia Onesimo kuwa huru.

C. Uchanganuzi:
   1. Ni vyema kuwa na imani na kuwaeleza wengine.
   2. Ni jambo jema kustahili imani toka kwa wengine.
   3. Injili ya Kristo hutokomeza utumwa (linga. Math.7:12).

XIII. “…Uniwekee mahali pa kukaa…” mstari wa 22.

A. Paulo anamwomba Filemoni aandaye nyumba ya kulala.

B. Hivyo basi anaamini kwamba muda si mrefu angemwona Filemoni (Linga. Filp.2:19-24).

C. Kufikia hapa Paulo anaomba sala kutoka kwa Filemoni.

D. Uchanganuzi:
   1. Kuna nguvu katika sala. Kama Paulo alihitaji sala za wengine, basi ni kiasi gani sisi tunahitaji sala za wengine.
   2. “Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii” (Yak.5:16).

XIV. Epafra, mstari wa 23.

A. Paulo anapeleka salaam za Epafra.

B. Anamtaja Epafra kuwa “aliyefungwa pamoja nami katika Kristo.”

C. Linganisha Kol.1:7; Kol.4:12.
1. Epafra alikuwa mwenyeji wa Kolosai, na inawezekana kupitia yeye kanisa lilianzishwa hapo.
2. Alikuwa ni mtumwa (bondservant) wa Yesu Kristo.

XV. “…Watendao kazi pamoja nami” mstari wa 24.

A. Hapa Paulo anawataja Marko, Aristarko, Dema, na Luka. Anawaita hawa “watenda kazi pamoja naye.”

B. Linga. Kol.4:10,14. Paulo hapa anawataja haswa: Aristarko, Marko, na mtu aliyeitwa Yesu wa Yusto, na Epafra (ambaye alikuwa mshiriki wa kanisa la Kolosai). Luka alikuwa pamoja naye; Dema alikuwa pamoja naye wakati huo; lakini wakati wa 2 Tim.4:9-11 Dema alikuwa amemwacha; Luka peke yake alikuwa pamoja naye.

XVI. Sala ya mwisho, mstari wa 25.

A. Paulo anaomba neema ya Bwana iwe juu ya Filemoni.

B. Ni kawaida katika nyaraka za Paulo kuhitimisha namna hii. “Neema ya Bwana Yesu Kristo na iwe pamoja na roho zenu. Ameni”

## KITABU CHA FILEMONI KWA UFUPI

Katika salaam Paulo amejitambulisha kuwa ni mwandishi, na kuwataja anaowaandikia na kusema maamkizi yenye sala. Paulo anataja “msingi wa shukrani” katika sala zake kwa Filemoni, na kurejea katika “msingi wa haja.” Anataja furaha nyingi na faraja ambavyo hupatikana katika upendo wa Filemoni. Kufuatia mwenendo uliongozwa na upendo, Paulo alimsihi Filemoni kwa niaba ya Onesmo.

Paulo anafafanua kwa kina hisia na kumjali kwake Onesimo. Anatoa rejea maalum kudhihirisha majaliwa ya Mungu katika kukutana kwake na Onesimo, na kumsihi Filemoni “kumpokea.” Paulo anakubaliwa kudaiwa yeye badala ya Onesimo iwapo kulikuwa na deni lolote. Kwa upole anamkumbusha Filemoni deni lake la kiroho kwa Paulo. Anamwomba sana Filemoni kufanya kama alivyoombwa, na kuonyesha imani kwamba Filemoni angefanya zaidi ya alivyoombwa, na kueleza kwamba alitazamia kumtembelea Filemoni muda si mrefu. Anatuma salaam kutoka kwa Epafra, na kumtaja kuwa “mtenda kazi pamoja naye,” na kutoa sala ya mwisho.

## MASOMO YA ZIADA KATIKA FILEMONI

1. Kuona mema kwa wengine kwa Paulo imekuwa dhahiri katika kitabu hiki kifupi. Katika Rum.12:17 Paulo hupendezwa, “Kuangalia yaliyo mema machoni pa watu wengine.” Katika 2 Kor.8:20,21 anasema, “Tukijiepusha na neno hili, mtu asije akatulaumu kwa habari ya karama hii tunayoitumikia; tukitangulia kufikiri yaliyo mema, si mbele za Bwa tu, ila na mbele ya wanadamu.” Alitamani kubaki na Onesimo, lakini asingefanya hivyo bila idhini ya Filemoni. Paulo asingemshurutisha Filemoni, bali alitaka afanye kwa hiari.

2. Somo kubwa lililobainishwa katika kitabu hiki ni ukweli kwamba toba huleta masahihisho (kurekebisha mambo) kwa kadiri iwezekanavyo ili kutenda haki. Onesimo, mtumwa, aliyekimbia kutoka kwa Filemoni, bwana wake. Alijifunza injili, na kufanyika kuwa Mkristo. Toba yake ya kweli ingemfanya arejee nyumbani, kwa bwana wake na kurekebisha mambo.

3. Kitabu cha Filemoni kinatoa rejea ya mafundisho ya Biblia juu ya majaliwa ya Mungu (providence). Paulo anasema, (mstari wa 15): Maana, labda ndiyo sababu alitengwa nawe kwa muda, ili uwe naye tena milele." Maelezo hayo ni sawa na Mordekai yaliyoandikwa katika Esta 4:14 – "…lakini ni nani ajuaye kama wewe hukuujia ufalme kwa ajili ya wakati kama huu?"

4. Katika kitabu cha Filemoni tunajifunza jambo jinsi injili ilivyomaliza tatizo la utumwa (ambao kimsingi ulifanywa na ufalme wa Rumi). Injili haikuamuru mara moja watumwa kuachwa huru. Hilo lingechochea mateso makali zaidi. Injili iliweka kanuni takatifu (kwa watumwa na mabwana zao) wapi na mahali gani pa kutumia, ingeufikisha mwisho utumwa. Mahali ambapo watu hupenda kuwatendea wengine jinsi ile ambayo wangependa wengine kuwatendea HAPATAKUWA NA UTUMWA KABISA HAPO!

5. Mtu Filemoni anasimama kama mfano bora (1) katika kuwa wakili Mkristo, (2) katika kulijali kanisa, (3) katika upendano wa ndugu, na (4) katika ushawishi wa Mkristo. Upendo wake mwingi na imani (1) mbele za Bwana Yesu Kristo, na (2) mbele za watakatifu wote.

6. Paulo alimwandikia Filemoni, kwa niaba ya Onesimo. Kama Onesimo alikuwa na mwingine (Paulo mwenyewe) wa kumwombea daawa lake, mithili ya jinsi alivyofanya mwingine (Kristo mwenyewe) kutuombea daawa letu. Yohana anasema, "Na kama mtu akitenda dhambi, tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki; naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu; bali na kwa dhambi za ulimwengu wote" (1 Yoh.2:1,2). Neno mwombezi (advocate) limetafsiriwa kutoka Kiyunani PARAKLATOS, lenye maana aliyeitwa kututetea upande wetu, kuisimamia daawa yetu – Mshauri upande wa utetezi.

7. Filemoni na Onesimo ni mfano wa upatanisho. Upande wa Onesimo, upatanisho ungehitaji toba ya kweli. Upande wa Filemoni, upatanisho ungehitaji msamaha wa kweli. Maudhui ya Biblia ni upatanisho – upatanisho baina ya mwanadamu na Mungu. Mungu ametekeleza na kutoa mpango mkamilifu ambao kwa huo upatanisho unawezekana. Mungu yuko tayari na anapenda kusamehe. Na anaagiza watu wa kila mahali "watubu" (Mdo.17:30). Mungu amefanya upande wake; mwanadamu ni lazima afanye upande wake!

8. Waraka huu unatufundisha upendo wa kweli wa Mkristo, huruma, na kujali wengine. Ingawa Paulo alikuwa katika hali ngumu, lakini alikuwa akiwafikiria wengine, na kufanya kazi siku zote kwa ajili ya wengine. Kwa njia ya kipekee na upendo alipenda kumsaidia rafiki yake na Mkristo mwenzake, Onesimo.

9. Paulo alimwambia hivi Filemoni, kuhusu Onesimo, "Na kama amekudhulumu, au unamwia kitu, ukiandike hicho juu yangu. Mimi Paulo nimeandika kwa mkono wangu mwenyewe, mimi nitalipa. Sikuambii kwamba nakuwia hata nafsi yako" (Film.18,19). Ndiyo kusema Onesimo ni mfano wa wanadamu wote. Watu wote kwa sababu ya dhambi zao wamemkosea aliyewamiliki. Wanadamu wote wana deni kwa Mungu, deni ambalo hawawezi kulilipa! Mfano wa Paulo, Bwana wetu amesema, "Niandikie mimi deni hilo, nitalilipa!" Bwana atalipa deni la kila mtu atakayemwamini yeye, na kutii mapenzi yake. Atafanya upatanisho kamili kabisa.

   Paulo anasema: "Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba Mungu anasihi kwa vinywa vyetu; twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu" (2 Kor.5:20).